



**NAWEZAJE KUWA MKULIMA
ALİYETHIBITISHWA**



1

Je, uthibitisho wa kilimo-hai ni lazima?

Shamba linaweza kuthibitishwa kulingana na viwango vya kilimo-hai vilivyopo. Hii hutokea pale mkulima anapotimiza masharti ya viwango na kuthibitishwa na mamlaka ya uthibitisho.

Kwa nini ni muhimu?



Kumsaidia mkulima kupata masoko ya bidhaa za kilimo-hai



Kutoa taarifa kwa wateja kwamba bidhaa inatokana na kilimo-hai na chanzo kinafahamika



Kuonyesha kwamba shughuli za kilimo haziharibu mazingira




Kuonyesha kwamba wafanyakazi wanatendewa vyema na hakuna mtoto aliyeajiriwa shambani

2

Ni nani anaweza kuthibitishwa kama Mkulima wa kilimo-hai?

Ni shamba ndilo linalothibitishwa na sio mkulima. Shamba hilo linapaswa kusimamiwa na mkulima huyo huyo ama katika eneo moja au maeneo mengi.

Kwa mfano:



Mkulima mwenye shamba moja linalozalisha zao moja au mazao mengi



Mkulima mwenye mashamba mengi yanayozalisha mazao mengi

Uthibitisho utahusisha maeneo yafuatayo:

- Maeneo yote yanayolimwa pamoja na maeneo yasiyolimwa, maeneo ya malisho ya mifugo
- Malighafi inayotumika katika kilimo (idadi yake na ilikotengenezwa)
- Shughuli zote zinazofanywa baada ya kuvuna kama vile kusafisha, kufungasha
- Ghala kwa ajili ya mazao na pembejeo
- Zana na vifaa vinavyotumika

Kwa habari zaidi kuhusu uthibitisho wa kilimo-hai, wasiliana na Shirika la Taifa la Kukuza na Kuendeleza Kilimo-hai (NOAM) katika nchi yako.

Nawezaje kuthibitishwa?

Ili aweze kuthibitishwa, mkulima atahitajika kutimiza hatua zifuatazo.

Katika Mwaka wa Kwanza:



Hatua 1: Soma habari kuhusu viwango na habari nyingine kutoka Shirika lako la Taifa la Kilimo-hai.



Hatua 2: Ulizia habari kutoka katika Mamlaka za Uthibitisho zilizopo. Wasiliana na Mamlaka na upate habari kuhusu viwango, mchakato wa maombi, gharama za uthibitisho, na taratibu.



Hatua 3: Chagua Mamlaka ya Uthibitisho inayofaa. Jeza na wasilisha maombi, jadiliana nao gharama za uthibitisho, taratibu na malipo ya ada. Weka saini mkataba wa ukaguzi na uthibitisho na Mamlaka hiyo.

Hatua 4: Tayarisha kumbukumbu za shamba. Andaa kumbukumbu za ramani za shamba kwa matayarisho ya ukaguzi wa shamba



Hatua 6: Jadili ripoti ya ukaguzi na Mkaguzi. Soma ripoti kwa uangalifu na kagua iwapo ina makosa yoyote au haieleweki.



Hatua 5: Ukaguzi wa shamba. Panga na Mamlaka ya Uthibitisho lini mkaguzi atakuja kukagua shughuli za shamba na kumbukumbu.

Hatua 7: libu maswali yote kutoka kwa mkaguzi. Kagua na timiza masharti yote yanayohitajika kwa ajili ya uthibitisho wako



Hatua 8: Uamuzi wa uthibitisho. Mamlaka ya uthibitisho hatimaye itakutaarifu matokeo ya ukaguzi na uamuzi wa uthibitisho.

4

Nawezaje kuendeleza uthibitisho wangu?

Shamba lako litakaguliwa kila mwaka na Mamlaka ya Uthibitisho. Hakikisha masharti yote ya uthibitisho kutoka kwenye Mamlaka ya Uthibitisho yanatimizwa.

Kwa hiyo, unapaswa kufanya yafuatayo:




Fanya marekebisho yaliyoagizwa, wakati vivango vikibadilishwa



Weka kumbukumbu zako zote vizuri zikiwa na taarifa za sasa



Hudhuria mafunzo kuhusu kilimo-hai ili kuboresha maarifa yako



Linda shamba la kilimo-hai lisichafuliwe na viambato visivyo asilia

Huu ni mwongozo wa msingi wa jinsi mkulima anavyoweza kuthibitishwa. Kwa habari zaidi wasiliana na Shirika lako la Kilimo-hai katika anuani zifuatazo:



BOAM

P.O Box 2251, Bujumbura - Burundi
Tel +25779910345
Email:sibad53@gmail.com



NOGAMU

Plot 957 Galukande Close, Off Tank Hill Road, Muyenga, P. O. Box 70071, Clock Tower, Kampala, Uganda.
Tel: +256 312 264039
admin@nogamu.org.ug
www.nogamu.org.ug



Tanzania Organic Agriculture Movement

TOAM

Shaurlimoyo/Lindi Str, Marlam Towers Bldg, P.O. Box 70089, Dar es salaam, Tanzania
Tel: +255 732 975 799
toam@kilimohai.org www.kilimohai.org



KOAN

ICIPE Complex, Kasarani Road
P.O. Box 72461-00200 Nairobi, Kenya
Tel: +254 20 2610863
Email: koansecretariat@elci.org
www.koan.co.ke



ROAM

B.P. 6886 Kigali - Rwanda
Tel +250 788558027
Email: rwandaorganicmovement@gmail.com



IFOAM Head Office

Phone: +49 228 92650 10
Email: headoffice@ifoam.org
www.ifoam.org

Chapisho hili limetolewa kwa ufadhili wa:



Swedish International Development
Cooperation Agency